JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2023

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2023

# KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO


DIBAJI .......... iv

1.0 UTANGULIZI .......... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA .......... 2

2.1 SEHEMU A: Kusikiliza Hadithi, Lugha ya Kifasihi, na Sarufi .......... 2

2.2 SEHEMU B: Utungaji .......... 50

2.3 SEHEMU C: Ufahamu .......... 56

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI .......... 66

4.0 HITIMISHO .......... 68

5.0 MAPENDEKEZO .......... 68

KIAMBATISHO NA. 1: Ufaulu wa Watahiniwa katika PSLE 2023 .......... 70

KIAMBATISHO NA. 2: Ulinganifu wa Ufaulu wa Watahiniwa katika PSLE 2022 na PSLE 2023 .......... 72

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2023 katika somo la Kiswahili. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa waliofanya mtihani huu kwa wanafunzi wanaosoma ngazi ya elimu ya msingi, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla. Taarifa hii inaonesha umahiri walionao watahiniwa katika kujibu maswali na changamoto zilizowakabili. Aidha, taarifa inaonesha umahiri uliojibiwa vizuri zaidi na kutoa mapendekezo kwa umahiri ambao watahiniwa wamepata changamoto katika kujibu maswali.

Katika taarifa hii uchambuzi wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umefanyika kwa kutumia maelezo, Chati, Jedwali, na Vielelezo. Mambo mbalimbali yaliyochangia watahiniwa kujibu vizuri maswali ya mtihani yamebainishwa. Mambo hayo ni pamoja na watahiniwa kuelewa matakwa ya maswali husika na kuwa na maarifa ya kutosha katika Vipengele vya umahiri vya somo la Kiswahili vilivyopimwa katika mtihani. Usahihi wa majibu yaliyotolewa na watahiniwa ni ushahidi kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili ulifanyika vizuri. Aidha, watahiniwa wachache walishindwa kutambua matakwa ya baadhi ya maswali, walichagua jibu zaidi ya moja au kutokuchagua jibu lolote.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, mrejesho huu utatoa hamasa kwa wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua stahiki ili kuboresha zaidi ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki ipasavyo katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Kiswahili ulikuwa na maswali arobaini na tano (45). Maswali arobaini (swali la 1 - 40) yalikuwa ya kuchagua jibu sahihi na kila swali lilikuwa na alama moja (1). Maswali matano (41 - 45) yalikuwa ya kujibu kutokana na habari iliyosomwa na Mtanihiwa na kila swali lilikuwa na alama mbili (2). Maswali hayo yaligawanywa katika sehemu A, B, na C. Sehemu A ilihusu Kusikiliza Hadithi, Lugha ya Kifasihi, na Sarufi. Sehemu hiyo ilikuwa na alama thelathini na tano (35). Sehemu B ilihusu Utungaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kukamilisha barua kwa kuchagua herufi iliyomo katika kisanduku na kujaza katika fomu ya OMR na ilikuwa na alama tano (5). Aidha, sehemu C ilihusu ufahamu ambapo mtahiniwa aliulizwa maswali mafupi matano (5) yaliyotokana na matini aliyopewa.

Jumla ya watahiniwa 1,397,293 walisajiliwa kufanya Mtihani wa somo la Kiswahili ambapo watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 97.06 walifanya mtihani. Watahiniwa 1,192,184 sawa na asilimia 87.91 walifaulu mtihani huu.

Taarifa hii ya uchambuzi imeonesha majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kila swali kwa kuzingatia idadi na asilimia ya watahiniwa waliochagua kila chaguo katika swali la 1-40. Aidha, kwa swali la 41- 45 uchambuzi umeonesha watahiniwa walioweza kujibu kwa usahihi na walioshindwa pamoja na changamoto katika kujibu maswali husika.

Majibu ya watahiniwa yalifanyiwa uchambuzi kwa kutumia viwango vya ufaulu katika madaraja matatu kama ifuatavyo: asilimia 60 - 100 ni daraja la kiwango kizuri cha ufaulu, asilimia 40 - 59 ni daraja la kiwango cha wastani cha ufaulu na asilimia 0 - 39 ni daraja la kiwango hafifu cha ufaulu. Alama ya nyota (*) katika chati na majedwali imetumika kuonesha herufi ya jibu sahihi. Vilevile, takwimu za watahiniwa ambao, ama walichagua jibu zaidi ya moja au hawakujibu swali, zimeoneshwa kwa kutumia neno “Mengine” katika majedwali na chati za uchambuzi. Aidha, rangi ya kijani, njano na nyekundu kwenye chati na majedwali zinawakilisha kiwango kizuri, wastani na hafifu cha ufaulu mtawalia.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulijikita katika kuangalia uwezo wa watahiniwa katika kujibu maswali husika. Aidha, uchambuzi huu unabainisha sababu za watahiniwa kujibu kwa usahihi maswali husika. Vilevile, uchambuzi huu unaelezea sababu ya watahiniwa kushindwa kujibu kwa usahihi maswali katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi.

Katika mtihani huu watahiniwa walifanya vizuri sana katika swali la 3 ambalo lilikuwa na asilimia 92.91. Kwa upande mwingine, swali la 44 lilikuwa na ufaulu wa chini zaidi kuzidi maswali yote kwa kuwa na asilimia 24.13.

## 2.1 SEHEMU A: Kusikiliza Hadithi, Lugha ya Kifasihi, na Sarufi

Sehemu hii ilikuwa na maswali thelathini na tano (35). Maswali matano (1-5) yalipima umahiri wa kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza ambapo mtahiniwa alitakiwa kusikiliza hadithi na kujibu maswali. Swali la 6 - 35 yalipima umahiri wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma. Watahiniwa walitakiwa kusikiliza hadithi ifuatayo kisha wajibu maswali yanayofuata:

*Baraka ni kijana aliyeishi bila wazazi. Wazazi wake walifariki kwa ajali ya ndege. Alilelewa na bibi yake mzaa baba aitwaye Bibi Mwema. Alikuwa mjukuu wa pekee wa Bibi Mwema. Baraka ni kijana mwenye nidhamu ya hali ya juu. Kila siku aliamka mapema ili kumsaidia bibi yake kazi za nyumbani kisha alijiandaa kwenda shuleni.*

*Baraka alipomaliza Elimu ya Msingi, bibi yake alipata maradhi. Baraka hakuwa na fedha ya kumpeleka bibi yake hospitali. Mungu si athumani, alipata kibarua cha kufyatua matofali. Alipata pesa ya kumtibia bibi yake. Baada ya muda kupita hali ya bibi yake ilitengemaa na Baraka aliendelea na masomo ya sekondari. Baraka alisoma kwa bidii na kufaulu vizuri mitihani yake. Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha Dodoma kusomea kozi ya udaktari.*


*Baraka alipohitimu masomo yake alirudi kijijini na kuwa Mganga Mkuu wa Zahanati. Anatibu watu kutoka kijijini kwao na vijiji vya jirani. Wanakijiji wanampenda sana Daktari Baraka. Wao wanamuona kama lulu kwao kwa sababu amekuwa msaada mkubwa sana kijijini.*

Baada ya watahiniwa kusikiliza hadithi waliyosomewa walitakiwa kujibu swali la 1-5 kwa lengo la kupima uelewa wao kuhusu hadithi hiyo:

**Swali la 1:** Nini kilisababisha kifo cha wazazi wake Baraka?

- A Uhaba wa hospitali kijijini
- B Ajali ya ndege
- C Maisha ya anasa ya wazazi wake
- D Ajali ya gari
- E Maisha duni ya wazazi wake

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha chanzo cha kifo cha wazazi wake Baraka kwenye hadithi aliyoisikiliza. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 1 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 1**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo


Chati Na. 1 inaonesha kuwa asilimia 92.72 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu B *Ajali ya ndege*. Watahiniwa hao walielewa vyema maudhui ya hadithi hiyo ambayo inahusu maisha ya Baraka baada ya kufiwa na wazazi wake, hivyo waliweza kubaini chanzo cha kifo cha wazazi wake Baraka.

Hata hivyo, asilimia 7.28 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi *A Uhaba wa hospitali kijijini,* C *Maisha ya anasa ya wazazi wake,* D *Ajali ya gari na* E *Maisha duni ya wazazi wake.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *uhaba wa hospitali kijijini* walishindwa kubaini kuwa, hali ya huduma za afya katika kijiji alichoishi Baraka haikuzungumziwa katika hadithi. Vilevile, waliochagua kipotoshi *maisha ya anasa* na *maisha duni ya wazazi wake*; hawakuelewa maudhui ya hadithi husika kuwa, haikuelezwa hali za maisha ya wazazi wake Baraka bali hadithi ilielezea maisha ya Baraka baada ya kufiwa na wazazi wake. Aidha, uchaguzi wa kipotoshi *ajali ya gari* haukuwa sahihi kwani katika hadithi ajali ya gari haikubainishwa bali ilibainishwa ajali ya ndege. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na umahiri wa kusikiliza na kuelewa hadithi waliyosomewa, hivyo kushindwa kubaini chanzo cha kifo cha wazazi wake Baraka.

**Swali la 2:** Nani alimlea Baraka baada ya kufiwa na wazazi wake?

A Wanakijiji
B Bibi yake mzaa mama
C Bibi yake mzaa baba
D Walimu wake
E Mganga Mkuu wa Zahanati

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha mtu aliyemlea Baraka baada ya kufiwa na wazazi wake. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 2 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 2**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 2 inaonesha kuwa asilimia 82.84 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi C *Bibi yake mzaa baba.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusikiliza na kuelewa maudhui ya hadithi waliyosomewa na msimamizi. Hivyo, waliweza kutambua kuwa Baraka alilelewa na *Bibi yake mzaa baba* baada ya kufiwa na wazazi wake.


Hata hivyo, asilimia 17.16 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A *Wanakijiji,* B *Bibi yake mzaa mama*, D *Walimu wake,* na *E Mganga Mkuu wa Zahanati.* Uchaguzi wa kipotoshi *wanakijiji* haukuwa sahihi kwa sababu hawakushiriki katika malezi ya Baraka bali wao walikuwa wanufaika wa kazi yake ya udaktari. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *bibi yake mzaa mama* haukuwa sahihi kwani mhusika huyo hakutajwa katika hadithi. Waliochagua kipotoshi *walimu wake,* walishindwa kutofautisha majukumu ya mzazi/mlezi ambaye humpatia mtoto mahitaji muhimu na mwalimu ambaye huwapatia watu elimu au maarifa fulani. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *Mganga Mkuu wa Zahanati* ulitokana na kushindwa kutambua kuwa hicho kilikuwa cheo alichopata Baraka baada ya kuhitimu masomo yake ya udaktari.

Uteuzi wa vipotoshi hivyo kwa ujumla unaonesha kuwa, watahiniwa hawakuwa makini katika kusikiliza hadithi hiyo wakati ikisomwa, jambo lililowafanya kukosa maarifa ya kutosha katika kujibu swali hili.

**Swali la 3:** Baraka alipataje fedha za kumpeleka bibi yake hospitali?

A Aliomba kwa wanakijiji
B Alifanya kibarua cha kufyatua matofali
C Alipewa na walimu wake
D Alipata kutoka vijiji vya jirani
E Alipewa na mganga mkuu

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mazingira ambayo Baraka alipata fedha za kumpeleka bibi yake hospitali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 3 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 3**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 3 inaonesha kuwa asilimia 92.91 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu sahihi B *Alifanya kibarua cha kufyatua matofali*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa


kusikiliza hadithi na kuelewa maudhui yaliyomo ndani ya hadithi hivyo, kuweza kujua kazi ya kufyatua matofali ndio ilimpa Baraka kipato cha kumtibia bibi yake alipougua.

Hata hivyo, asilimia 7.09 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A *Aliomba kwa wanakijiji*, C *Alipewa na walimu wake,* D *Alipata kutoka vijiji vya jirani*, na E *Alipewa na mganga mkuu.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *aliomba kwa wanakijiji* walishindwa kuelewa kuwa Baraka alikuwa mchapakazi na alikuwa akijishughulisha na kazi mbalimbali ikiwemo kufyatua matofali. Waliochagua kipotoshi *alipewa na walimu wake* walishindwa kuelewa maudhui ya hadithi husika kwani katika hadithi hiyo haikubainisha kama fedha aliyoipata Baraka kuwa, alipewa na walimu wake. Aidha, waliochagua kipotoshi *alipata kutoka vijiji vya jirani* walishindwa kuelewa kuwa Baraka alikuwa anatibu watu kutoka vijiji vya jirani baada ya kuajiriwa kama daktari na sio kupewa fedha kutoka katika vijiji hivyo. Vilevile, waliochagua kipotoshi *alipewa na mganga mkuu*, walishindwa kuelewa kuwa Baraka ndiye aliyekuwa mganga mkuu. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa, watahiniwa hawakuwa na umahiri katika kusikiliza na kuelewa maudhui ya hadithi hiyo, hali iliyosababisha kushindwa kuchagua jibu sahihi la swali husika.

**Swali la 4:** Baraka alisoma kozi gani baada ya kuhitimu masomo ya sekondari?

A Uashi
B Urubani
C Uuguzi
D Udereva
E Udaktari

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha kozi aliyosoma Baraka alipojiunga na Chuo Kikuu cha Dodoma baada ya kuhitimu masomo ya sekondari. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 4 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 4**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 4 inaonesha kuwa asilimia 91.94 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu sahihi *E Udaktari*, kozi aliyosomea Baraka baada ya kuhitimu elimu ya sekondari. *Jambo* linaloonesha kuwa watahiniwa walikuwa na umahiri wa kusikiliza hadithi na kuelewa maudhui.


Hata hivyo, asilimia 8.06 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A *Uashi,* B *Urubani,* C *Uuguzi* na D *Udereva.* Uchaguzi wa kipotoshi *uashi* haukuwa sahihi kwa sababu Baraka hakujihusisha na kazi ya ujenzi kwa kutumia matofali au mawe bali alifyatua matofali pekee. Waliochagua kipotoshi *urubani* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kozi hii inayompa mtu uwezo wa kuendesha au kuongoza chombo kama vile *ndege* au *kuwa mwanahewa*. Pia, waliochagua kipotoshi *uuguzi* walishindwa kutofautisha taaluma ya uuguzi na udaktari. Watahiniwa hao hawakujua kuwa uuguzi ni taaluma ya jinsi ya kutoa huduma ya kiafya kwa mgonjwa lakini udaktari ni elimu ya utabibu kwa mgonjwa. Aidha, waliochagua kipotoshi *udereva* hawakuelewa kuwa kozi hiyo ilihusu ujuzi wa kuendesha vyombo vinavyosafiri nchi kavu. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha ya kuelewa maudhui ya hadithi husika. Kwani majibu hayo hayahusiani

na kazi aliyosomea Baraka ya kutibu wagonjwa katika hospitali au zahanati (udaktari).

**Swali la 5:** Kwa nini wanakijiji walimuona Baraka ni lulu kwao?

A Alifaulu vizuri mitihani yake
B Alikuwa msaada mkubwa sana kijijini
C Aliwapa pesa nyingi
D Alifyatua matofali na kuwapatia
E Alifanya biashara na kuwanufaisha

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha sababu iliyowafanya wanakijiji kumuona Baraka kuwa ni lulu kwao. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 5 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 5**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Takwimu katika chati Na. 5 zinaonesha kuwa asilimia 87.99 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi B *alikuwa msaada mkubwa sana kijijini*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha ya kusikiliza hadithi waliyosomewa, hivyo kuelewa vyema maudhui yaliyomo. Kwa hiyo, waliweza kutambua kuwa sababu iliyomfanya Baraka


kuonekana kuwa wa muhimu zaidi kijijini ilikuwa ni huduma ya kitabibu aliyoitoa kwa wanakijiji pamoja na vijiji vya jirani, hivyo kuwa msaada mkubwa sana kwao.

Hata hivyo, asilimia 12.01 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A *alifaulu vizuri mitihani yake,* C *aliwapa pesa nyingi,* D *alifyatua matofali na kuwapatia na* E *alifanya biashara na kuwanufaisha.* Uchaguzi wa kipotoshi *alifaulu vizuri mitihani yake,* ulitokana na watahiniwa kushindwa kuelewa maudhui ya hadithi hivyo, kuhusianisha na kitendo cha kufanya vizuri mitihani na sifa nzuri za Baraka za kufanya kazi kwa weledi kuwa ni sababu ya Baraka kuwa lulu kwao. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *aliwapa pesa nyingi* hawakuelewa kuwa Baraka hakuwapa pesa bali alitoa huduma ya kitabibu kijijini na vijiji vya jirani. Aidha, uchaguzi wa kipotoshi *alifyatua matofali na kuwapatia* hawakuelewa kwamba hicho kilikuwa kibarua alichofanya Baraka katika jitihada za kupata fedha kwa ajili ya kumuuguza bibi yake. Vilevile, waliochagua kipotoshi *alifanya biashara na kuwanufaisha* walishindwa kuelewa maudhui yaliyomo kwenye hadithi. Kwani katika msuko wa matukio katika hadithi husika hakuna sehemu ambayo mtunzi alielezea kuhusu Baraka kujihusisha na biashara. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kusikiliza na kuelewa maudhui ya hadithi. Hivyo, walishindwa kubainisha sababu sahihi iliyomfanya Baraka kuonekana lulu kwa wanakijiji.

**Swali la 6:** “Jino langu linang’aa.” Wingi wa sentensi hii ni upi kati ya sentensi zifuatazo?

A Meno zangu yanang’aa.
B Meno yangu linang’aa.
C Meno yangu yanang’aa.
D Majino yangu yanang’aa.
E Jino zangu zinang’aa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 6 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 6**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 6 inaonesha kuwa asilimia 78.96 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu sahihi *C Meno yangu yanang'aa*. Watahiniwa hao waliweza kuonesha uhusiano uliopo kati ya nomino, kivumishi na kitenzi katika wingi wa sentensi *jino langu linang'aa*.


Kwa upande mwingine, asilimia 21.05 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A *Meno zangu yanang'aa,* B *Meno yangu linang'aa,* D *Majino yangu yanang'aa*, na E *Jino zangu zinang'aa.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa walikosa umahiri katika kutumia upatanisho wa kisarufi katika sentensi zenye hali ya wingi. Kwa mfano, uteuzi wa kipotoshi *meno zangu yanang'aa* ulitokana na watahiniwa hao kushindwa kubaini kuwa kivumishi 'zangu' hakiwezi kupatana kisarufi na nomino *meno* katika wingi. Vivyo hivyo, katika kipotoshi *meno yangu linang'aa* hawakujua kuwa neno 'linang'aa' linapatana kisarufi na neno *jino* katika umoja. Pia, uteuzi wa kipotoshi *majino yangu yanang'aa* ulitokana na kushindwa kutambua kuwa neno 'majino' sio wingi wa neno jino bali ni *meno*. Hali kadhalika, uchaguzi wa kipotoshi *jino zangu zinang'aa* ulitokana na watahiniwa kukosa uelewa wa upatanisho wa kisarufi katika maneno hayo yasiyo na uhusiano wowote katika umoja au wingi.

Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu upatanisho wa kisarufi wa sentensi katika hali ya umoja na wingi.

**Swali la 7:** “Manamba angalimsikiliza baba yake ________ mguu”. Neno lipi kati ya yafuatayo linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A Asingeliumia
B Angaliumia
C Asingaliumia
D Asingeumia
E Angeliumia

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 7 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 7**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 7 inaonesha kuwa asilimia 51.16 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu sahihi C *asingaliumia*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kuelewa matumizi ya upatanisho wa kisarufi. Hivyo, waliweza kubaini muundo sahihi wa sentensi. Aidha,

waliweza kuelewa kuwa kama sehemu moja ya sentensi shurutia ikiundwa na viambishi shurutishi **-ngali-** ni lazima upande wa pili wa sentensi hiyo ukamilishwe na viambishi shurutishi hivyo katika vitenzi. Pia, waliweza kubaini kuwa neno hilo lazima liwe na ukanushi -si- kutokana na muktadha wa sentensi husika.

Hata hivyo, asilimia 48.84 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A *asingeliumia* B *angaliumia* D *asingeumia, na E angeliumia*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *asingeliumia* hawakubaini kuwa neno hilo halina upatanisho wa kisarufi -ngali- kama ilivyotumika katika neno walilopewa. Pia, waliochagua kipotoshi *angaliumia* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo halina ukanushi *-si-* tofauti na Muktadha wa sentensi. Vilevile, waliochagua kipotoshi *asingeumia* hawakubaini kuwa neno hilo halina upatanisho sahihi wa kisarufi -ngali- kama ilivyotakiwa. Aidha, waliochagua kipotoshi *angeliumia* hawakuelewa kuwa kipotoshi hiki hakina upatanisho wa kisarufi *-ngali-* na pia neno hilo halina ukanushi *-si-* kwa kuzingatia sentensi iliyotolewa. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi.


Swali la 8 hadi 19 yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali,* hususan umahiri mahususi wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 8:** Makuli walisikika wakisema, “Kidole kimoja hakivunji chawa.” Je, ni methali ipi kati ya zifuatazo inafanana na methali hiyo?

A Mchonga mwiko huukimbiza mkono wake.
B Chanda chema huvishwa pete.
C Kidole chako kibaya kitakufaa siku mbaya.
D Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.
E Kidole chako kibaya usikikate.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutambua maana na matumizi ya methali mbalimbali. Kiwango cha

ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 8 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 8**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 8 inaonesha kuwa asilimia 66.17 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu sahihi D *Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali mbalimbali kwani walibaini kwa usahihi methali inayofanana na methali "kidole kimoja hakivunji chawa" ambayo inasisitiza ushirikiano katika kufanya kazi.


Hata hivyo, asilimia 33.83 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A *Mchonga mwiko huukimbiza mkono wake,* B *Chanda chema huvishwa pete,* C *Kidole chako kibaya kitakufaa siku mbaya, na* E *Kidole chako kibaya usikikate.* Uchaguzi wa kipotoshi *mchonga mwiko huukimbiza mkono wake* hakikuwa sahihi kwa sababu methali hii inatoa tahadhari wakati wa kufanya kazi ili kuepuka jambo baya linaloweza kutokea na haisisitizi ushirikiano katika kufanya kazi. Pia, uchaguzi wa kipotoshi *chanda chema huvishwa pete* ulitokana na watahiniwa hao kutokujua kuwa methali hiyo inasisitiza kupewa pongezi kwa mtu aliyefanya jambo vizuri. Aidha,

vipotoshi *kidole chako kibaya kitakufaa siku mbaya* na *kidole chako kibaya usikikate* vilichaguliwa bila kujua kuwa methali hizo zinasisitiza kutokudharau au kutupilia mbali vitu visivyo na manufaa kwa sasa ambavyo huenda vikafaa kwa siku zijazo. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali mbalimbali za Kiswahili.

**Swali la 9:** "Tunashauriwa kuwalea watoto katika maadili mema." Methali ipi kati ya zifuatazo inaendana na kauli hiyo?

A Ugambi ni wa wenye ndumba
B Udongo uwahi ungali maji
C Tone na tone hujaza ndoo
D Tone na tone huwa mchirizi
E Ubishi mwingi huvuta matendo

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kubaini maana na matumizi ya methali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 9 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 9**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 9 inaonesha kuwa asilimia 49.79 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu sahihi B *Udongo uwahi ungali maji.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maana, matumizi na busara zilizopo katika methali mbalimbali. Hivyo waliweza kubaini kwa usahihi kuwa malezi ya watoto kuhusu maadili mema hupaswa kufanywa mapema wangali wadogo ili kujenga jamii bora.


Kwa upande mwingine, asilimia 50.21 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A *Ugambi ni wa wenye ndumba,* C *Tone na tone hujaza ndoo,* D *Tone na tone huwa mchirizi* na E *Ubishi mwingi huvuta matendo*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ugambi ni wa wenye ndumba* hawakuelewa kuwa methali hiyo ina maana ya majigambo ya watu wanaotenda mambo ya kijasiri. Uchaguzi wa vipotoshi *tone na tone hujaza ndoo* na *tone na tone huwa mchirizi*; zenye maana sawa na methali isemayo *haba na haba hujaza kibaba* zinasisitiza uwekaji wa akiba. Hivyo, inaonesha kwamba watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa methali hizo hazina uhusiano na malezi na maadili. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *ubishi mwingi huvuta matendo* unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa methali hiyo ina maana ya matendo hukidhi haja kuliko maneno ambapo ni kinyume na matakwa ya swali.

Uteuzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa mahiri katika kutumia methali na maana zake katika tungo za kifasihi kwani maana zilizopo katika vipotoshi hivyo hazina uhusiano na malezi na maadili kwa watoto.

**Swali la 10:** “Kisongo alipoumia Kajiru alimpeleka hospitali kwa matibabu. Methali ipi kati ya zifuatazo ingefaa kutumiwa na Kisongo kwa jambo alilotendewa na Kajiru?

A Asiyekubali kushindwa si mshindani
B Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli
C Shukurani ya punda ni mateke
D Hakuna marefu yasiyo na ncha
E Mtaka cha uvunguni sharti ainame

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya methali katika tungo za kifasihi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 10 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 10**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 10 inaonesha kuwa asilimia 74.89 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu sahihi *B Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali. Hivyo, waliweza kubaini kwa usahihi methali inayoweza kutumika kuashiria tendo la huruma linalofanywa na mtu kwa aliyepatwa na matatizo.


Hata hivyo, asilimia 25.11 ya watahiniwa walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua kati ya vipotoshi A *Asiyekubali kushindwa si mshindani* C *Shukurani ya punda ni mateke,* D *Hakuna marefu yasiyo na ncha* na E *Mtaka cha uvunguni sharti ainame.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *asiyekubali kushindwa si mshindani* hawakuelewa kuwa methali hii huwasihi binadamu kukubali wakishindwa au kuukiri udhaifu wao. Uchaguzi wa kipotoshi *shukurani ya punda ni mateke* hawakujua kuwa methali hiyo huwakosoa watu wasiotoa shukurani baada ya kupewa

msaada fulani. Aidha, waliochagua kipotoshi *hakuna marefu yasiyo na ncha* hawakuelewa kuwa methali hiyo hutumika kumliwaza mtu mwenye matatizo; na uteuzi wa kipotoshi *mtaka cha uvunguni sharti ainame* ulitokana na watahiniwa hao kutokuelewa kuwa methali hiyo huwakumbusha watu kuwa tayari kukisumbukia kitu wanachokitaka. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa hao kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana na ujumbe unaopatikana katika methali husika, hivyo kujibu swali hilo kinyume na matakwa ya swali.

**Swali la 11:** Wao walikuwa hawana furaha. Neno "wao" lipo katika nafsi ipi kati ya hizi zifuatazo?

A Nafsi ya tatu wingi
B Nafsi ya pili wingi
C Nafsi ya tatu umoja
D Nafsi ya kwanza wingi
E Nafsi ya pili umoja

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kufahamu nafsi na mazingira ya utokeaji wake katika sentensi mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 11 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 11**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo


Chati Na. 11 inaonesha kuwa asilimia 50.82 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu sahihi A *Nafsi ya tatu wingi.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu neno *wao* ambalo limetumika katika sentensi hiyo kudhirisha nafsi ya tatu wingi.

Hata hivyo, asilimia 49.18 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi B *Nafsi ya pili wingi,* C *Nafsi ya pili umoja,* D *Nafsi ya kwanza wingi* na E *Nafsi ya pili umoja.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *nafsi ya pili wingi* walishindwa kuelewa kuwa nafsi hiyo huwakilishwa na neno "ninyi/nyinyi". Pia, waliochagua *nafsi ya tatu umoja* hawakujua kuwa huwakilishwa na neno "yeye". Vilevile, waliochagua kipotoshi *nafsi ya kwanza wingi* hawakuelewa kuwa nafsi hiyo huwakilishwa na neno "sisi" na waliochagua *nafsi ya pili umoja* hawakuelewa kuwa nafsi hiyo huwakilishwa na neno "wewe". Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kubaini viwakilishi vya nafsi katika umoja na uwingi na jinsi zinavyotumika katika sentensi za lugha ya Kiswahili.

**Swali la 12:** ''Alivyoendelea kukanusha ________ hasira zilivyozidi kumpanda yule askari.'' Neno lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A ndipo
B ndiko
C ndivyo
D ndio
E ndiyo

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 12 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 12**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 12 inaonesha kuwa asilimia 49.56 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi *C ndivyo*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi katika kuandika sentensi zenye kuonesha namna au jinsi ya kutenda jambo. Aidha,


waliweza kubaini kuwa neno “ndivyo” ni kitenzi kishirikishi kipatanishi kinachodokeza hali inayodhihirika katika viumbe hai.

Hata hivyo, asilimia 50.44 ya watahiniwa walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili, walichagua kati ya vipotoshi A *ndipo* B *ndiko* D *ndio, na E ndiyo*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndipo* hawakuelewa kuwa neno hilo ni kitenzi kishirikishi kinachodokeza mahali ambapo ni karibu. Pia waliochagua kipotoshi *ndiko* hawakuelewa kuwa neno hilo linatumika kudokeza mahali ambapo ni mbali. Vilevile, waliochagua kipotoshi *ndio* hawakuelewa kuwa neno hilo hutumika kuonesha kitenzi kishirikishi kwa viumbe hai. Kadhalika, waliochagua kipotoshi *ndiyo* hawakujua kuwa neno hilo ni kitenzi kishirikishi kipatanishi kinachotumika kudokeza hali ya kukubali jambo. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi husika.

**Swali la 13:** Nikitoka bustanini nitawapikia watoto chakula. Neno “nitawapikia” lipo katika kauli gani?

A Kutendwa
B Kutendeana
C Kutendea
D Kutendana
E Kutendewa

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa katika matumizi ya kauli mbalimbali za vitenzi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 13 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 13**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 13 inaonesha kuwa asilimia 53.02 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi C *Kutendea*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika kutumia kauli mbalimbali za vitenzi na kubaini kuwa, kauli ya kutendea huoneshwa na kiambishi **–e-** au **–i-** kama kinavyoonekana kwenye kitenzi "nitawapikia" katika sentensi waliyopewa inayotokea baada ya mzizi na kabla ya kiambishi tamati maana.

Kwa upande mwingine, asilimia 46.98 ya watahiniwa walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili, walichagua kati ya vipotoshi A *Kutendwa*, B *Kutendeana*, D *Kutendana E Kutendewa*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kutendwa* walishindwa kuelewa kuwa hiyo ni kauli inayodhihirika kwa upachikaji wa kiambishi –**w**- baada ya mzizi na kabla ya kiambishi tamati maana. Waliochagua kipotoshi *kutendeana* walishindwa kuelewa kuwa kauli hiyo huoneshwa kwa upachikaji wa kiambishi –**ean**- baada ya mzizi wa neno. Pia, waliochagua kipotoshi *kutendana* hawakuelewa kuwa kauli hiyo huoneshwa kwa upachikaji wa kiambishi –**an**- baada ya mzizi na kabla ya kiambishi tamati maana. Aidha, kipotoshi *kutendewa* hakikuwa sahihi kwani kauli hii hutokana na upachikwaji wa

kiambishi –**ew-** baada ya mzizi na kabla ya kiambishi tamati maana katika shina la neno. Kwa ujumla, watahiniwa hao walionesha kukosa umahiri katika kutumia kauli mbalimbali za vitenzi vya Kiswahili.

**Swali 14:** Mwalimu wa somo la Kiswahili alipigwa na butwaa baada ya kuambiwa mwanafunzi wa Darasa la Saba ameacha shule. Nahau "pigwa butwaa" ina maana gani?

A Kukubaliana
B Kushangaa
C Kufurahi
D Kuchukizwa
E Kukataa

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kubaini maana za nahau katika tungo za kifasihi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 1 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 1: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 41,717 | 1,114,563 | 48,941 | 96,469 | 46,711 | 7,830 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 3.08 | 82.18 | 3.61 | 7.11 | 3.44 | 0.58 |

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa watahiniwa 1,114,563 sawa na asilimia 82.18 walichagua jibu sahihi B *Kushangaa*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maana na matumizi ya nahau "pigwa butwaa" kuwa ni hali ya kushangaa baada ya kusikia au kuona kitu fulani.

Hata hivyo, watahiniwa 241,668 sawa na asilimia 17.82 walichagua kati ya vipotoshi A *Kukubaliana,* C *Kufurahi*, D *Kuchukizwa*, na E *Kukataa*. Uchaguzi wa kipotoshi *kukubaliana* watahiniwa hawakujua

kuwa neno hilo lina maana kuridhia jambo. Waliochagua kipotoshi *kufurahi* hawakuelewa kuwa hiki ni kitendo cha kukunjua moyo au kuchangamka au kuridhika. Pia, waliochagua kipotoshi *kuchukizwa* hawakuelewa kuwa ni kitendo cha kufanyiwa jambo la kuudhi. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *kukataa* ulitokana na kutokujua kuwa neno hilo lina maana ya kutokukubaliana na jambo au tendo fulani. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa mahiri katika kutumia nahau na maana zake katika tungo za kifasihi.

**Swali la 15:** Juhudi za Suli kufanya kazi serikalini ziligonga mwamba baada ya kukosa cheti cha kumaliza Elimu ya Msingi. Nahau "gonga mwamba" katika sentensi hii ina maana gani?

A Kufika mwisho kabisa
B Kupasua mwamba mgumu
C Kufika kikomo
D Kufanya jambo bila mafanikio
E Kupata suluhu ya kazi

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kubaini maana za nahau katika tungo za kifasihi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 2 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 2: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 265,000 | 78,422 | 286,395 | 638,220 | 79,527 | 8,667 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 19.54 | 5.78 | 21.12 | 47.06 | 5.86 | 0.64 |

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa watahiniwa 638,220 sawa na asilimia 47.06 walichagua jibu sahihi D *Kufanya jambo bila mafanikio*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu

maana na matumizi ya nahau “gonga mwamba” kuwa ni hali ya kufanya jambo bila kupata mafanikio.

Hata hivyo, watahiniwa 718,011 sawa na asilimia 52.94 walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili walichagua kati ya vipotoshi A *Kufika mwisho kabisa, B Kupasua mwamba mgumu*, C *Kufika kikomo*, *na* E *Kupata suluhu ya kazi*. Uteuzi wa kipotoshi *kufika mwisho kabisa* ulitokana na watahiniwa kutokubaini kuwa kufika mwisho kwa jambo ni kukamilika kwa jambo. Aidha, uchaguzi wa kipotoshi *kupasua mwamba mgumu,* watahiniwa hawakujua kuwa hicho ni kitendo cha kufanya mwamba kuwa vipande. Kipotoshi *kufika kikomo,* watahiniwa hawakuelewa kuwa hii ni hali/wakati/mahali pa kumalizia. Pia, waliochagua kipotoshi *kupata suluhu ya kazi* walishindwa kuelewa kuwa ni hali ya kupata ufumbuzi wa jambo. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa mahiri katika kutumia nahau na maana zake katika tungo za kifasihi.

**Swali la 16:** Tabia ya wanafunzi kuchelewa shuleni imeota mizizi. Nahau “ota mizizi’’ ina maana gani?

A Kufanikiwa kufika shuleni
B Kujificha ili wasionekane
C Kustawi na kudumu sana
D Kupenda kuishi shuleni
E Kutodumu kwa muda mrefu

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kubaini maana na matumizi ya nahau katika tungo za kifasihi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 3 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 3: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi.ya Watahiniwa** | 106,315 | 269,489 | 722,965 | 57,524 | 189,354 | 10,584 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 7.84 | 19.87 | 53.31 | 4.24 | 13.96 | 0.78 |

Jedwali Na. 3 linaonesha kuwa watahiniwa 722,965 sawa na asilimia 53.31 walichagua jibu sahihi C *Kustawi na kudumu sana*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maana na matumizi ya nahau "ota mizizi" kuwa ni hali ya kustawi na kudumu sana.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 633,266 sawa na asilimia 46.69 walichagua kati ya vipotoshi A *Kufanikiwa kufika shuleni*, B *Kujificha ili wasionekane*, D *Kupenda kuishi shuleni*, na E *Kutodumu kwa muda mrefu*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi *kufanikiwa kufika shuleni*, *kujificha ili wasionekane* na *kupenda kuishi shuleni*, walishindwa kuelewa kuwa vipotoshi hivyo havihusiani na jambo linaloonekana kufanyika kwa muda mrefu. Aidha, waliochagua kipotoshi *kutodumu kwa muda mrefu* walishindwa kuelewa kuwa ni kauli inayokinzana na nahau "ota mizizi" yaani kustawi na kudumu sana. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri katika kutumia nahau na maana zake katika tungo za kifasihi.

**Swali la 17:** Neno jumuishi linaloundwa kutokana na maneno "kuku, njiwa, kunguru na bata'' ni lipi?

A Wadudu
B Ndege
C Mboga
D Wanyama
E Kitoweo

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutumia msamiati katika kuwasiliana. Kiwango cha ufaulu katika

swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 4 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 4: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 34,877 | 1,148,664 | 41,822 | 67,026 | 55,918 | 7,924 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 2.57 | 84.70 | 3.08 | 4.94 | 4.12 | 0.58 |

Jedwali Na. 4 linaonesha kuwa watahiniwa 1.148,664 sawa na asilimia 84.70 walichagua jibu sahihi B *Ndege* ambalo lina maana ya kiumbe mwenye mabawa na manyoya ambaye aghalabu huruka angani. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kujua msamiati mbalimbali inayoundwa kutokana na maneno jumuishi ya majina yaliyotajwa kwenye swali husika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 207,567 sawa na asilimia 15.3 walichagua kati ya kipotoshi A *Wadudu,* C *Mboga,* D *Wanyama*, na E Kitoweo. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *wadudu* hawakubaini kuwa maana ya neno hilo ni viumbe wadogo na bila ya uti wa mgongo. Uchaguzi wa kipotoshi *mboga* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana ya majani yanayoliwa na binadamu aghalabu baada ya kupikwa. Vilevile, waliochagua kipotoshi *wanyama* walishindwa kuelewa kuwa ni viumbe wenye uhai wenye miguu. Sambamba na hayo, uteuzi wa kipotoshi *kitoweo* ulitokana na kutokuelewa kuwa neno hilo hujumuisha mchuzi, mboga, samaki au nyama kinachotumika kulia chakula. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kufahamu msamiati mbalimbali inayoundwa na maneno jumuishi.

**Swali la 18:** Chikoyo alihuzunika sana aliposikia taarifa ya kifo cha Babu yake. Katika neno ‘’aliposikia’’ kiambishi kipi huwakilisha wakati uliopita?

A a-
B -po-
C -sik-
D -ki-
E -li-

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutumia njeo mbalimbali katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 5 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na.5: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 257,191 | 163,208 | 159,685 | 54,296 | 709,438 | 12,413 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 18.96 | 12.03 | 11.77 | 4.00 | 52.31 | 0.92 |

Jedwali Na. 5 linaonesha kuwa watahiniwa 709,438 sawa na asilimia 52.31 walichagua jibu sahihi E ***-li-*** kwa sababu huelezea wakati uliopita ambao Chikoyo alihuzunika sana. Aidha, viambishi vya wakati hutokea katika vitenzi vikuu vya sentensi.

Hata hivyo, watahiniwa 646,793 sawa na asilimia 47.69 walichagua kati ya vipotoshi A *a-*, B *-po-*, C *-sik-* na D *-ki-.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *a-* hawakuelewa kuwa kiambishi hicho hudokeza nafsi ya tatu umoja. Pia, waliochagua kipotoshi *-po-* hawakuelewa kuwa hicho ni kiambishi rejeshi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *-sik-* walishindwa kuelewa kuwa ni sehemu ya mzizi wa neno. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *-ki-* walishindwa kuelewa kuwa ni silabi ya tano katika neno husika ambayo haina

kazi maalum ya kusarufi. Kwa ujumla watahiniwa hao walishindwa kubaini njeo ya wakati uliopita katika kitenzi walichopewa.

**Swali la 19:** “Mwanafunzi alicheza vizuri. ’’Ukanushi wa sentensi hii ni upi?

A Mwanafunzi hakucheza vizuri.
B Mwanafunzi hakuchezaga vizuri.
C Mwanafunzi hatacheza vizuri.
D Mwanafunzi hucheza vizuri.
E Mwanafunzi hajacheza vizuri.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima dhana ya ukanushi katika nyakati mbalimbali katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 6 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 6: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 955,544 | 78,030 | 90,799 | 122,174 | 100,773 | 8,911 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 70.46 | 5.75 | 6.69 | 9.01 | 7.43 | 0.66 |

Jedwali Na. 6 linaonesha kuwa watahiniwa 955,544 sawa na asilimia 70.46 walichagua jibu sahihi A *Mwanafunzi hakucheza vizuri.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya ukanushi katika wakati uliopita ambapo huundwa na kiambishi -ku- katika kitenzi kulingana na muktadha wa sentensi husika.

Hata hivyo, watahiniwa 400,687 sawa na asilimia 29.54 walichagua kati ya vipotoshi B *Mwanafunzi hakuchezaga vizuri,* C *Mwanafunzi hatacheza vizuri,* D *Mwanafunzi hucheza vizuri*, na E *Mwanafunzi hajacheza vizuri.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *Mwanafunzi hakuchezaga vizuri*, hawakuelewa kuwa silabi ‘ga’ iliyoongezwa

mwishoni mwa kitenzi iliitokana na athari za lugha za kikabila. Pia, waliochagua kipotoshi *Mwanafunzi hatacheza vizuri* hawakuelewa kuwa sentensi hiyo hudokeza ukanushi wa sentensi katika wakati ujao. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *Mwanafunzi hucheza vizuri* hawakuelewa kuwa sentensi hii haidokezi ukanushi bali ni uyakinifu unaodokeza hali ya mazoea. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *Mwanafunzi hajacheza vizuri*, walishindwa kuelewa kuwa sentensi hii hudokeza ukanushi wa sentensi katika wakati timilifu. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutumia ukanushi wa matukio katika nyakati mbalimbali.

Swali la 20 hadi 25 yaliandaliwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali*, katika umahiri mahususi wa kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali.

**Swali la 20:** Maneno haya hayajapangwa katika utaratibu wa kialfabeti: “dada, kisu, andika, cheza, zuhura.’’ Yakipangwa kwa utaratibu wa kialfabeti seti sahihi itakuwa ipi kati ya zifuatazo?

A kisu, cheza, andika, zuhura, dada
B andika, cheza, dada, kisu, zuhura
C zuhura, cheza, dada, kisu, andika
D zuhura, kisu, dada, cheza, andika
E cheza, andika, kisu, dada, zuhura

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali hili lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutumia kamusi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 7 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 7: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 127,720 | 759,340 | 173,731 | 114,252 | 169,299 | 11,889 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 9.42 | 55.99 | 12.81 | 8.42 | 12.48 | 0.88 |

Jedwali Na. 7 linaonesha kuwa watahiniwa 759,340 sawa na asilimia 55.99 walichagua jibu sahihi *B andika, cheza, dada, kisu, zuhura*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kubaini mpangilio sahihi wa herufi za alfabeti za Kiswahili kwa kutumia kamusi.

Hata hivyo, watahiniwa 596,891 sawa na asilimia 44.01 walichagua kati ya vipotoshi A *kisu, cheza andika, zuhura, dada,* C *zuhura, cheza, dada, kisu, andika*, D *zuhura, kisu, dada, cheza, andika* na E *cheza, andika, kisu, dada, zuhura.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kubaini mpangilio wa herufi za alfabeti za Kiswahili kwa kutumia kamusi. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa maneno *andika, cheza, dada, kisu, zuhura* yamepangwa kwa kufuata mpangilio wa alfabeti a, ch, d, k na z mtawalia.

**Swali la 21:** **"**Wanafunzi hupenda kula maharage." Sentensi hii ipo katika hali gani kati ya zifuatazo?

A Timilifu
B Uliopo
C Mazoea
D Uliopita
E Ujao

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutumia hali na nyakati mbalimbali za vitenzi katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 8 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 8: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 135,826 | 160,721 | 906,926 | 82,977 | 59,962 | 9,819 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 10.01 | 11.85 | 66.87 | 6.12 | 4.42 | 0.72 |

Katika Jedwali Na. 8 watahiniwa 906,926 sawa na asilimia 66.87 walichagua jibu sahihi *C mazoea*. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa kiambishi **hu-** katika kitenzi huelezea hali ya tendo linalofanyika mara kwa mara.

Hata hivyo, watahiniwa 449,305 sawa na asilimia 33.13 walishindwa kubaini kiambishi cha hali ya mazoea katika sentensi waliyopewa. Watahiniwa hao walichagua kati ya vipotoshi A *Timilifu,* B *Uliopo,* D *uliopita, na* E *Ujao*. Watahiniwa walichagua kipotoshi *timilifu* kwa kuwa walishindwa kuelewa kuwa hali timilifu hutumia kiambishi -me- katika kuelezea tendo. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *uliopo* walishindwa kubaini kuwa hudokeza hali ya wakati uliopo kwa kutumia kiambishi -na- katika kuelezea tendo na kipotoshi *uliopita* hawakujua kuwa hudokeza hali ya wakati uliopita inayotumia kiambishi -li- katika kuelezea tendo. Aidha, waliochagua kipotoshi *ujao* hawakubaini kuwa hali ya wakati ujao hutumia kiambishi -ta- katika kuelezea tendo. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kutumia hali na nyakati mbalimbali za matendo katika sentensi.

**Swali la 22:** Neno lipi linakamilisha sentensi isemayo, “Humo _____ alimoingia yule nyoka”?

A ndimo
B ndiyo
C ndipo
D ndiko
E siyo

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 9 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 9: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 983,220 | 89,268 | 180,255 | 50,902 | 43,765 | 8,821 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 72.50 | 6.58 | 13.29 | 3.75 | 3.23 | 0.65 |

Jedwali Na. 9 linaonesha kuwa watahiniwa 983,220 sawa na asilimia 72.50 walichagua jibu sahihi *A ndimo*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi katika kuandika sentensi zenye kuonesha mahali, watu au vitu vilipo. Aidha, waliweza kubaini kuwa neno “ndimo” ni kitenzi kishirikishi chenye maana ya kuwa ndani ya kitu, hivyo kukamilisha kwa usahihi sentensi husika.

Hata hivyo, watahiniwa 373,011 sawa na asilimia 27.5 walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili na kuchagua kati ya vipotoshi B *ndiyo* C *ndipo* D *ndiko, na E sipo*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndiyo* hawakuelewa kuwa neno hilo linatumika katika kukubali jambo. Vilevile, waliochagua vipotoshi *ndipo* na *ndiko* hawakujua kuwa maneno hayo hutumika kuonesha umbali na ukaribu wa vitu mtawalia. Aidha, waliochagua kipotoshi *sipo* hawakuelewa kuwa neno hilo hutumika kuonesha kitenzi kishirikishi kikanushi. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutumia upatanisho wa kisarufi katika sentensi za lugha ya Kiswahili.

**Swali la 23:** Neno lipi kati ya yafuatayo **halilandani** na maneno mengine?

A Mkunga
B Mchungaji
C Muuguzi
D Tabibu
E Daktari

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati kwenye lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 10 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 10: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 246,463 | 803,603 | 75,718 | 126,486 | 93,024 | 10,937 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 18.17 | 59.25 | 5.58 | 9.33 | 6.86 | 0.81 |

Jedwali Na. 10 linaonesha kuwa watahiniwa 803,603 sawa na asilimia 59.25 walichagua jibu sahihi B *Mchungaji.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya msamiati kulingana na miktadha mbalimbali. Hivyo, waliweza kubaini kuwa *mchungaji* ni mtu anayefanya kazi ya kupeleka wanyama wa kufugwa malishoni na kuwarudisha zizini/kiongozi katika madhehebu fulani ya Kikristo.

Hata hivyo, watahiniwa 552,628 sawa na asilimia 40.75 walioshindwa kujibu swali hili walichagua kati ya vipotoshi A Mk*unga,* C *Muuguzi,* D *Tabibu,* na E *Daktari.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi *mkunga, muuguzi, tabibu na daktari* walishindwa kuelewa maana na matumizi ya msamiati huo. Majina yote yana sifa inayofanana yaani wote ni wataalam wa afya wenye kutoa huduma za afya hospitalini ambapo; *mkunga* ni mtu mwenye ujuzi wa kuzalisha, *muuguzi* ni mtu mwenye ujuzi wa kuhudumia wagonjwa, *tabibu* ni mtu mwenye ujuzi wa kutibu wakati daktari ni mtu aliyehitimu elimu ya tiba ya dawa za kisasa. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo walikosa umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya msamiati katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 24:** “Mama alipata bahati ya kusalimiana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania” Neno lipi kati ya yafuatayo linaweza kutumika badala ya neno “bahati?”

A shani
B tunu
C fursa
D hiba
E wasaa

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa visawe vya maneno mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 11 linaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 11: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 106,937 | 123,539 | 921,896 | 70,020 | 123,348 | 10,491 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 7.88 | 9.11 | 67.97 | 5.16 | 9.09 | 0.77 |

Jedwali Na. 11 linaonesha kuwa watahiniwa 921,896 sawa na asilimia 67.97 walichagua jibu sahihi *C fursa.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu visawe vya maneno. Hivyo, waliweza kubaini maana ya neno hilo kuwa ni nafasi ya kuweza kufanya jambo.

Hata hivyo, watahiniwa 434,335 sawa na asilimia 32.03 walichagua kati ya vipotoshi A *shani*, B *tunu*, D hiba*,* na E *wasaa.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *shani* hawakuelewa kuwa *neno shani* ni jambo au kitu kinachoshangaza na ambacho si kawaida yake kutokea; *tunu* ni kitu anachopewa mtu mwingine kama ishara ya mapenzi; *hiba* ni mali anayopewa mtu kwa radhi ya upendo, na *wasaa* ni nafasi ya wakati anayokuwa nayo mtu kufanya jambo lingine lolote. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kuelewa visawe vya maneno mbalimbali.

**Swali la 25:** **“**Kaa anatembea upandeupande.” Katika sentensi hii neno “upandeupande” linatumika kama aina gani ya neno?

A Kivumishi
B Kiwakilishi
C Kielezi
D Nomino
E Kitenzi

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 12 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 12: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 249,300 | 209,516 | 656,118 | 114,363 | 114,159 | 12,775 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 18.38 | 15.45 | 48.38 | 8.43 | 8.42 | 0.94 |

Jedwali Na. 12 linaonesha kuwa watahiniwa 656,118 sawa na asilimia 48.38 walichagua jibu sahihi *C Kielezi*. Hii inadhihirisha kwamba watahiniwa hao walikuwa na uelewa juu ya “kielezi” kuwa huelezea zaidi kuhusu tendo lilivyotendeka. Hivyo, waliweza kubaini neno “upandeupande” kuwa ni kielezi kinachotoa taarifa zaidi kuhusu kitenzi *anatembea*.

Hata hivyo, watahiniwa 700,113 sawa na asilimia 51.62 walichagua kati ya vipotoshi *A Kivumishi, B Kiwakilishi, D Nomino* na *E Kitenzi*. Watahiniwa waliochagua kivumishi, walishindwa kutambua kuwa ni neno linalotoa taarifa zaidi kuhusu nomino. Pia, uteuzi wa kiwakilishi unatokana na watahiniwa kuhusisha neno “upandeupande” kama neno linalosimama badala ya nomino kimakosa. Vilevile, uteuzi wa

nomino umetokana na watahiniwa kuhusisha neno “upandeupande” kama nomino dhahania bila kujua kuwa nomino ni neno linalotaja majina ya watu, vitu au mahali. Aidha, uteuzi wa kitenzi ni ushahidi kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa kuwa hilo ni neno linaloarifu tendo linalofanyika. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno na matumizi yake katika sentensi za Kiswahili.

Swali la 26 hadi 30, maswali yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*, katika umahiri mahususi wa kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali.

**Swali la 26:** Upepo unaovuma kwa nguvu na kwa kasi, kiasi cha kubomoa majengo huitwaje?

A Ngurumo
B Radi
C Kimbunga
D Mvua
E Kipupwe

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati kwenye lugha ya Kiswahili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 13 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 13: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 63,207 | 108,200 | 1,002,205 | 64,625 | 108,832 | 9,162 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 4.66 | 7.98 | 73.90 | 4.77 | 8.02 | 0.68 |

Jedwali Na. 13 linaonesha kuwa watahiniwa 1,002,205 sawa na asilimia 73.90 walichagua jibu sahihi C *Kimbunga.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya msamiati

kulingana na miktadha mbalimbali. Hivyo, waliweza kubaini kimbunga ni upepo unaovuma kwa nguvu na kwa kasi, kiasi cha kuharibu miundo mbinu.

Hata hivyo, watahiniwa 354,026 sawa na asilimia 26.1 walichagua kati ya vipotoshi A *Ngurumo*, B *Radi*, D *Mvua* na E *Kipupwe*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ngurumo* hawakuelewa kuwa ngurumo sio upepo bali ni sauti kubwa na nzito inayotokana na kitu kama radi, gari, eropleni au mnyama kama vile simba. Kipotoshi *radi* hakikuwa sahihi kwani nayo ni sauti kubwa inayotoka mawinguni inayoambatana na mwanga mkubwa wakati wa mvua. Kadhalika, watahiniwa waliochagua kipotoshi *mvua* hawakujua haya ni matone ya maji yanayodondoka kutoka kwenye mawingu. Pia, uteuzi wa kipotoshi *kipupwe* ulitokana na watahiniwa kutokujua kuwa haya ni majira ya baridi yanayotokea katika miezi ya Juni, Julai na Agosti katika Afrika ya Mashariki. Kwa ujumla watahiniwa waliochagua vipotoshi hivi walikosa umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya msamiati katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 27:** **"**Mimi _____ mtoto mkubwa kwenye familia yetu". Ni neno lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A ndiyo
B ndiwe
C ndiye
D ndie
E ndio

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 14 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 14: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 216,581 | 51,763 | 840,636 | 103,343 | 134,796 | 9,112 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 15.97 | 3.82 | 61.98 | 7.62 | 9.94 | 0.67 |

Jedwali Na. 14 linaonesha kuwa watahiniwa 840,636 sawa na asilimia 61.98 walichagua jibu sahihi *C ndiye*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi katika kuandika sentensi zenye kuonesha mahali, watu au vitu vilipo. Aidha, waliweza kubaini kuwa neno “ndiye” ni kitenzi kishirikishi kinachotumika kwa binadamu/mnyama mmoja hivyo, hutoa maana iliyokamili katika sentensi husika.

Hata hivyo, watahiniwa 515,595 sawa na asilimia 38.02 walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili, walichagua kati ya vipotoshi A *ndiyo* B *ndiwe* D *ndie, na E ndio*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndiyo* hawakuelewa kuwa neno hilo linatumika katika kukubali jambo. Vivyo hivyo, uteuzi wa kipotoshi *ndio* hawakuelewa kuwa neno hilo halitumiki kuonesha kitenzi kishirikishi kwa binadamu. Aidha, uchaguzi wa vipotoshi *ndiwe* na *ndie* ulitokana na kutokuelewa kuwa maneno hayo siyo sanifu na hayana maana yoyote ya kisarufi katika lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutumia upatanisho wa kisarufi katika sentensi za lugha ya Kiswahili.

**Swali la 28:** “Yule mtoto nyumbani anakuja’’ Upi ni mpangilio sahihi wa maneno unaounda sentensi hii?

A Anakuja yule mtoto nyumbani
B Mtoto nyumbani yule anakuja
C Nyumbani yule mtoto anakuja
D Mtoto yule anakuja nyumbani
E Yule nyumbani anakuja mtoto

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika mpangilio sahihi wa maneno katika kuunda sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 15 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 15: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 92,265 | 51,738 | 47,986 | 1,122,381 | 35,694 | 6,167 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 6.80 | 3.81 | 3.54 | 82.76 | 2.63 | 0.45 |

Katika Jedwali Na. 15 watahiniwa 1,122,381 sawa na asilimia 82.76 walichagua jibu sahihi D *Mtoto yule anakuja nyumbani.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mpangilio sahihi wa maneno katika sentensi za Kiswahili. Hivyo, walielewa kuwa katika mpangilio wa maneno hayo ili sentensi ilete maana lazima tungo hiyo ianze na N+V+T+E.

Hata hivyo, watahiniwa 233,850 sawa na asilimia 17.24 walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili. Watahiniwa hao walichagua kati ya vipotoshi A *Anakuja yule mtoto nyumbani*, B *Mtoto nyumbani yule anakuja,* C *Nyumbani yule mtoto anakuja,* na E *Yule nyumbani anakuja mtoto*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *anakuja yule mtoto nyumbani* walishindwa kuelewa kuwa mpangilio huo sio sahihi kwa sababu kiarifu hakiwezi kuchukua nafasi ya kiima katika sentensi. Pia, waliochagua kipotoshi *mtoto nyumbani yule anakuja* walishindwa kuelewa kuwa kielezi “nyumbani” hakiwezi kutokea baada ya nomino katika upande wa kiima kwa kuzingatia muktadha wa sentensi husika. Vilevile, waliochagua kipotoshi *nyumbani yule mtoto anakuja* na *yule nyumbani anakuja mtoto* walishindwa kuelewa kuwa, muundo wa sentensi za Kiswahili huzingatia mpangilio maalum unaojengwa na kiima na kiarifu. Uchaguzi wa vipotoshi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kutumia aina za maneno kwa usahihi ili kuunda sentensi zilizo kamili.

**Swali la 29:** Neno lipi linaundwa kutokana na silabi "ondoko'' zilizochanganywa?

A Ndoo
B Kondoa
C Kondoo
D Ondoka
E Ondoa

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuunda neno kutokana na silabi zilizochanganywa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Jedwali Na. 16 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 16: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 47,987 | 63,059 | 1,064,570 | 125,313 | 47,818 | 7,484 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 3.54 | 4.65 | 78.49 | 9.24 | 3.53 | 0.55 |

Jedwali Na. 16 linaonesha kuwa watahiniwa 1,064,570 sawa na asilimia 78.49 walichagua jibu sahihi C *Kondoo*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu uundaji wa maneno mapya kwa kubadili mpangilio wa herufi na silabi. Watahiniwa hao walibaini kuwa mpangilio sahihi wa herufi zilizochanganywa "ondoko" unaunda neno *kondoo* lenye maana ya mnyama afugwaye mwenye manyoya marefu yatengenezwayo sufu.

Hata hivyo, watahiniwa 291,661 sawa na asilimia 21.51 walichagua kati ya vipotoshi A *ndoo*, B *Kondoa*, D *Ondoka, na* E *Ondoa*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi *ndoo* na *ondoa* hawakuwa na uelewa kuwa katika maneno hayo herufi "k" imedondoshwa. Pia, katika neno ondoa herufi "a" imeongezwa kinyume na herufi zilizochanganywa alizopewa katika swali husika. Kadhalika, katika uteuzi wa vipotoshi *kondoa* na *ondoka*, watahiniwa hawakubaini kuwa katika maneno hayo, herufi "a" haikuwepo katika herufi

alizopewa katika swali hili. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa uundaji wa maneno mapya kwa kubadili mpangilio wa herufi na silabi walizopewa katika swali husika.

**Swali la 30:** Nomino ipi imeundwa kutokana na kitenzi imba?

A kuimba
B wimbo
C imbika
D imbiwa
E imbisha

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuunda nomino kutokana na kitenzi alichopewa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Jedwali Na. 17 linaonesha idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 17: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika Kila Chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 246,551 | 739,113 | 141,565 | 89,851 | 127,796 | 11,355 |
| **Asimia ya Watahiniwa** | 18.18 | 54.50 | 10.44 | 6.63 | 9.42 | 0.84 |

Jedwali Na. 17 linaonesha kuwa watahiniwa 739,113 sawa na asilimia 54.50 walichagua jibu sahihi B *wimbo.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika uundaji wa maneno kutoka kitenzi kwenda nomino. Aidha, walibaini kuwa kitendo cha kuimba kimesababishwa na kuwepo kwa wimbo ambao ni nomino.

Hata hivyo, watahiniwa 617,118 sawa na asilimia 45.5 walichagua kati ya vipotoshi A *kuimba* C *imbika,* D *imbiwa*, na E *imbisha.* Watahiniwa hao walikosa maarifa kuhusu uundaji wa maneno kutoka kategoria moja ya neno kwenda kategoria nyingine kama swali lilivyotaka. Uchaguzi wa kipotoshi *kuimba* unaonesha kuwa hawakuelewa kuwa neno hilo ni kitenzi jina kilichopachikwa kiambishi awali *ku-.* Kadhalika*,* watahiniwa walichagua vipotoshi


*imbika*, *imbiwa* na *imbisha* kwani walishindwa kuelewa kuwa maneno hayo ni vitenzi vilivyopo katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendesha na yaliyopachikwa viambishi vya kauli baada ya mzizi na kabla ya kiambishi tamati ambavyo ni -ik-, -iw- na -ish- mtawalia. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kuunda nomino kutokana na kitenzi husika.

Swali la 31 hadi 33, maswali yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kuonesha Uelewa wa jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*, katika umahiri mahususi wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma.

**Swali la 31:** "Wanakijiji walisherehekea mwenge wa uhuru mpaka liamba." Nahau "mpaka liamba." kama ilivyotumika katika sentensi hii ina maana gani?

A Hadi usiku
B Hadi asubuhi
C Hadi machweo
D Hadi adhuhuri
E Hadi jioni

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kubaini maana za nahau katika tungo za kifasihi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Chati Na. 14 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 14**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo


Chati Na. 14 inaonesha kuwa asilimia 62.57 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A *Hadi usiku*, C *Hadi machweo,* D *Hadi adhuhuri na E Hadi jioni.* Uchaguzi wa kipotoshi *hadi usiku* ulitokana na kushindwa kubaini kuwa *usiku* ni kipindi baada ya kutua jua. Pia, uteuzi wa kipotoshi *hadi machweo* hawakujua kuwa *machweo* ni wakati jua linapozama. Vilevile, waliochagua kipotoshi *hadi adhuhuri* hawakuelewa kuwa *adhuhuri* ni wakati wa mchana kuanzia saa sita hadi saa tisa mchana. Aidha, waliochagua kipotoshi *hadi jioni* hawakuelewa kuwa huo ni wakati kutoka alasiri mpaka machweo ya jua. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa matumizi na maana ya nahau “mpaka liamba”.

Hata hivyo, asilimia 37.43 ya watahiniwa walijibu vizuri swali hili kwa kuchagua jibu sahihi B *Hadi asubuhi.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maana na matumizi ya nahau “mpaka liamba” kuwa ni hali ya kukesha usiku kucha bila kulala hadi asubuhi. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kuelewa matumizi ya nahau katika miktadha mbalimbali.

**Swali la 32:** “Ringa alipopata taarifa za kifo cha wazazi wake aliinika kichwa.” Je, Ringa alifanya nini kati ya vitendo vifuatavyo?

A Aliinamisha kichwa kwa huzuni
B Aliinua kichwa juu kwa huzuni
C Alitikisa kichwa kwa huzuni
D Aligonga kichwa kwa huzuni
E Alishika kichwa kwa huzuni

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutumia nahau katika miktadha mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 15 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 15**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo


Chati Na. 15 inaonesha kuwa asilimia 52.74 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi A*, Aliinamisha kichwa kwa huzuni.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa matumizi ya nahau katika tungo mbalimbali za Kiswahili. Hivyo, waliweza kubaini kwa usahihi maana ya nahau "inika kichwa" ni kufanya kichwa kielekee chini.

Hata hivyo, asilimia 47.26 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi B *Aliinua kichwa juu kwa huzuni*, C *Alitikisa kichwa kwa huzuni,* D *Aligonga kichwa kwa huzuni na* E *Alishika kichwa kwa huzuni*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *aliinua kichwa juu kwa huzuni* walishindwa kubaini ishara hiyo hutumika kuelezea kukubalika kwa jambo au kuomba dua. Uteuzi wa kipotoshi *alitikisa kichwa kwa huzuni* walishindwa kubaini kuwa ni hali ya kukataa jambo fulani. Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *aligonga kichwa kwa huzuni*, walishindwa kubaini kuwa neno hilo huonesha mtu kufikiria au kuvuta kumbukumbu juu ya jambo fulani. Vilevile, uteuzi wa kipotoshi *alishika kichwa kwa huzuni* hawakuelewa kuwa neno hilo huonesha kushtushwa na jambo. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya nahau "inika kichwa".

**Swali la 33:** “Alipofika kazini bila kutarajia alipewa barua ya kupandishwa cheo” Methali ipi ina maana sawa na maelezo hayo?

A Riziki kama ajali huitambui ijapo.
B Raha haiji ila baada ya taabu.
C Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
D Usiandikie mate angali wino upo.
E Tamaa mbele mauti nyuma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kubaini maana na matumizi ya methali katika tungo za kifasihi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 16 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 16**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 16 inaonesha kuwa asilimia 55.01 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi A *Riziki kama ajali huitambui ijapo.* Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maana, matumizi na busara zilizopo katika methali mbalimbali hivyo kubaini

kuwa mtu huwa haitambui riziki imjiapo kwani huweza kumjia ghafla kama ajali hususan kupandishwa cheo au kupata madaraka fulani.


Hata hivyo, asilimia 44.99 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi B *Raha haiji ila baada ya taabu, C Mgaagaa na upwa hali wali mkavu*, D *Usiandikie mate angali wino upo*, na E *Tamaa mbele mauti nyuma*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *raha haiji ila baada ya taabu* walishindwa kujua kuwa hii ni methali inayotia moyo watu wapatapo shida wanapaswa kupambana ili hatimaye kupata raha.

Uteuzi wa kipotoshi *mgaagaa na upwa hali wali mkavu* watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa methali hiyo husisitiza mtu anayehangaikia jambo fulani lazima mwishowe atafanikiwa. Aidha, waliochagua kipotoshi *usiandikie mate angali wino upo* hawakuelewa kuwa methali hiyo ina maana kuwa usibahatishe jambo wakati uwezo wa kuthibitisha upo. Kadhalika, waliochagua kipotoshi *tamaa mbele mauti nyuma* walishindwa kuelewa kuwa methali hiyo inamaana kuwa binadamu hutamani sana kuridhisha nafsi zao huku akisahau kuwa kuna kifo mbele. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa umahiri wa kutumia methali katika tungo za kifasihi kwani maana za methali katika vipotoshi hivyo hazina uhusiano na swali husika.

**Swali la 34:** "Nchi ya Tanzania ipo kusini _________ nchi ya kenya." Neno lipi kati ya yafuatayo linafaa kukamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A mwa
B ya
C kwa
D wa
E na

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi mbalimbali. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 17 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 17**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo


Chati Na. 17 inaonesha kuwa asilimia 81.94 ya watahiniwa waliojibu swali hili walichagua jibu sahihi A *mwa*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi katika kuandika sentensi zenye kuonesha vihusishi kati ya nomino na nomino au nomino na kivumishi. Hivyo, waliweza kubaini kuwa neno "mwa" ni kihusishi sahihi kinachokamilisha maana ya sentensi katika swali husika.

Hata hivyo, asilimia 18.06 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi B *ya,* C *kwa,* D *wa*, na *E na*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi "ya" na "wa" hawakuelewa kuwa hivyo ni vihusishi vya kivumishi cha A-unganifu, na kipotoshi *kwa* ni kihusishi cha utumizi kama kifaa au chombo. Wakati kipotoshi *na* ni neno linalofanya kazi ya kiunganishi. Kwa ujumla watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi kulingana na miktadha mbalimbali.

**Swali la 35:** "Juakali anatembea kwa maringo _______ ya kinyonga." Jibu lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A mithili
B kwa sababu
C kwa kuwa
D mfano
E kinyume

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika matumizi ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 18 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 18**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 18 inaonesha kuwa asilimia 63.52 ya watahiniwa waliojibu swali hili walichagua jibu sahihi A *mithili*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi katika kuandika sentensi zenye kutumia viunganishi kati ya nomino na nomino au nomino na kivumishi. Hivyo, waliweza kubaini kuwa neno "mithili" ni kiunganishi linganifu kinachokamilisha maana ya sentensi katika swali husika.

Hata hivyo, asilimia 36.48 ya watahiniwa walichagua vipotoshi B *kwa sababu,* C *kwa kuwa,* D *mfano*, na E *kinyume.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi *kwa sababu* na *kwa kuwa* hawakuelewa kuwa ni viunganishi visababishi; wakati kipotoshi *mfano* ni kiunganishi linganifu kisichokidhi upatanisho wa kisarufi katika sentensi husika. Vilevile, uchaguzi wa kipotoshi *kinyume* hawakuelewa kuwa neno hilo hufanya kazi ya kutofautisha jambo

moja na lingine na siyo ulinganifu kama ulivyo muktadha wa swali husika. Hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutumia viunganishi katika upatanisho wa kisarufi kulingana na miktadha mbalimbali.

## 2.2 SEHEMU B: Utungaji

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano (36 - 40) yaliyohusu barua rasmi. Watahiniwa walitakiwa kukamilisha barua waliyopewa kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku. Swali lilikuwa kama ifuatavyo:

Kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku, kamilisha barua ifuatayo kwa kujibu swali la 36 - 40 kwa **kuweka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi** katika fomu yako ya kujibia.

| |
|---|
| A N. Puyanga B YAH: MAOMBI YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA<br>C Mkuu wa Shule D 22/12/2023 E Neema Puyanga |

Kijiji cha Nyankoronko,
S.L.P 27,
Rukwa.
36. __________

37. __________________
Shule ya Sekondari Sinzieni,
S.L.P 11,
Singida.

Ndugu,

38. ____________________________________

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.
Mimi ni mwanafunzi niliyemaliza Elimu ya Msingi mwaka 2023 katika shule ya msingi Nyankoronko. Nimefaulu vizuri Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi katika masomo yangu yote sita na kupata wastani wa alama B. Naomba kujiunga na masomo ya Kidato cha Kwanza katika shule yako. Naambatanisha na nakala ya matokeo yangu ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi.

Nitafurahi iwapo ombi langu litakubaliwa.

Ni mimi mtiifu,

39__________________

40__________________


Katika kujibu maswali haya, watahiniwa walitakiwa kukamilisha kifungu cha habari kama ifuatavyo**:**

| 36 | 37 | 38 | 39 | 40 |
|---|---|---|---|---|
| D | C | B | A | E |

Uchambuzi wa kina wa majibu ya watahiniwa katika kila swali (36-40) ni kama ifuatavyo:

**Swali la 36:**

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuandika barua rasmi kwa kuonesha tarehe katika anuani ya mwandishi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 19 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.





**Chati Na. 19**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 19 inaonesha kuwa asilimia 81.55 ya watahiniwa waliojibu swali hili walichagua jibu sahihi D *22/12/2023*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo na mpangilio wa vipengele vya uandishi wa barua rasmi. Hivyo, waliweza kubaini kuwa *tarehe* ndiyo inayokaa chini ya anuani ya mwandishi katika uandishi wa barua rasmi kwenye swali husika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua machaguo yasiyo sahihi walikosa stadi ya utungaji wa barua rasmi. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuhusu uandishi wa barua rasmi hivyo, kushindwa kubaini kuwa *tarehe* ndiyo inayokaa chini ya anuani ya mwandishi.

**Swali la 37:**

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kuhusu barua rasmi aliyopewa kwa kuonesha anayepelekewa barua. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 20 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.





**Chati Na. 20**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 20 inaonesha kuwa asilimia 60.56 ya watahiniwa waliojibu swali hili walichagua jibu sahihi C *Mkuu wa Shule*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo na mpangilio wa vipengele vya uandishi wa barua rasmi. Hivyo, waliweza kubaini kuwa anuani ya mwandikiwa kwenye barua rasmi hutaja cheo cha mpelekewa barua ambaye ni *Mkuu wa Shule*.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua machaguo yasiyo sahihi walikosa maarifa kuhusu uandishi wa barua rasmi. Hivyo, kushindwa kubaini kuwa anuani ya mwandikiwa kwenye barua rasmi hutaja cheo cha mpelekewa barua ambaye ni *Mkuu wa Shule.*

**Swali la 38**:

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kukamilisha barua rasmi aliyopewa kwa kuandika kichwa cha barua. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 21 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 21**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo


Chati Na. 21 inaonesha kuwa asilimia 72.78 ya watahiniwa waliojibu swali hili walichagua jibu sahihi B *YAH: MAOMBI YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA*. Watahiniwa hao waliweza kubaini kwa usahihi wa kichwa cha barua kwa kuwa huandikwa kwa herufi kubwa, hukaa katikati mwanzoni mwa barua na hubeba lengo la barua husika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua machaguo yasiyo sahihi walikosa maarifa kuhusu uandishi wa barua rasmi. Hivyo,

kushindwa kubaini kuwa kichwa cha barua huandikwa kwa herufi kubwa na hukaa katikati mwanzoni mwa barua.

**Swali la 39:**

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kubaini sehemu inapowekwa saini ya mwandishi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Chati Na. 22 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 22**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo


Chati Na. 22 inaonesha kuwa asilimia 35.87 ya watahiniwa waliojibu swali hili walichagua jibu sahihi A *N. Puyanga*. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa barua rasmi lazima iwe na saini ya mwandishi ambapo jina la kwanza huandikwa kwa kifupi na jina linalofuata huandikwa kwa ukamilifu. Pia, walibaini kuwa saini hiyo ya mwandishi hutokea mwishoni mwa barua kabla ya jina la mwandishi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wengi hawakuwa na maarifa kuhusu uandishi wa barua rasmi. Hivyo, walichagua kipotoshi E

Neema Puyanga kwani watahiniwa hao, hawakuwa na uelewa kuwa saini hukaa kabla ya jina la mwandishi.

**Swali la 40:**

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kukamilisha barua rasmi aliyopewa kwa kuonesha jina la mwandishi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Chati Na. 23 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




**Chati Na. 23**: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo

Chati Na. 23 inaonesha kuwa asilimia 33.36 ya watahiniwa waliojibu swali hili walichagua jibu sahihi E *Neema Puyanga*. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa mwishoni mwa barua rasmi lazima kuwe na jina la mwandishi linalokaa chini ya saini ya mwandishi na kuandikwa kwa ukamilifu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua machaguo yasiyo sahihi walikosa maarifa kuhusu uandishi wa barua rasmi. Hivyo, walishindwa kubaini kuwa mwishoni mwa barua rasmi lazima kuwe na jina la mwandishi linalokaa chini ya saini ya mwandishi.

## 2.3 SEHEMU C: Ufahamu

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano (41 - 45) kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo alilosoma* hususan umahiri mahususi wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma. Mtahiniwa alitakiwa kusoma kwa makini na kuelewa kifungu cha habari kisha kujibu maswali kutokana na habari hiyo. Aidha, katika sehemu hii uchambuzi unaonesha watahiniwa waliofanya vizuri ni wale waliopata alama kuanzia moja hadi mbili na walioshindwa kujibu vizuri ni wale waliopata alama sifuri. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa.


*Ukataji wa miti umekuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira. Binadamu hufyeka miti kwa lengo la kupata mkaa, kufanya shughuli za kilimo, kuchana mbao, kujenga nyumba na mahitaji mengine mengi. Hapa Tanzania ukataji miti umefanywa kwa kiasi kikubwa sana hasa miaka ya hivi karibuni.*

*Binadamu amediriki hata kukata miti na kuchoma majani pembezoni mwa vyanzo vya maji. Ukataji wa miti kwenye vyanzo vya maji umekuwa ukisababisha madhara kadha wa kadha kama vile: kukauka kwa vyanzo vya maji na ukosefu wa mvua kwa muda mrefu. Endapo binadamu ataendelea na uharibifu huo kwa muda mrefu madhara mengine mengi yanaweza kujitokeza.*

*Licha ya binadamu kutambua madhara ya ukataji wa miti ovyo hususani kwa kupitia vyombo vya habari, bado amekuwa* ***akibeza*** *ushauri huo unaotolewa na wataalamu wa mazingira na kuendelea na uharibifu. Hii inakumbusha wahenga walivyosema "****sikio la kufa halisikii dawa****." Kutokana na uharibifu huo maeneo mengi ya nchi yamekuwa yakikosa mvua za uhakika na mara nyingi hupata dhoruba zenye madhara makubwa kwa binadamu na makazi yao. Hivyo watu wanashauriwa kupanda miti, kuacha kuchoma mkaa na kuchoma majani pembezoni mwa vyanzo vya maji.*


**Swali la 41:** Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari kinachofaa kulingana na habari aliyoisoma. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 24 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila alama.





**Chati Na. 24**: Asilimia ya watahiniwa katika kila alama

Chati Na. 24 inaonesha kuwa asilimia 75.83 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na umahiri wa kusoma na kuelewa maudhui ya kifungu cha habari hivyo waliandika kwa usahihi kichwa cha habari *UHARIBIFU WA MAZINGIRA/UKATAJI WA MITI*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na umahiri wa kutosha kwa kuandika kichwa cha habari kilichozingatia vigezo vyote muhimu kama vile kutumia herufi kubwa, idadi ya maneno yasiyozidi matano na kuzingatia mawazo makuu yaliyomo katika habari husika. Kielelezo Na.1 kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa aliyepata alama zote za swali hili.




**Kielelezo Na. 1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 41*

Aidha, watahiniwa 327,750 sawa na asilimia 24.17 walishindwa kuandika kichwa cha habari kwa usahihi kutokana na kukosa umahiri katika kusoma na kuelewa maudhui ya kifungu cha habari. Baadhi yao walishindwa kubaini mawazo makuu katika habari husika. Wengine waliandika kichwa cha habari kisichoendana na habari waliyopewa. Aidha, walitumia herufi ndogo badala ya herufi kubwa kama kanuni za uandishi wa kichwa cha Habari zinavyoelekeza. Kwa mfano, baadhi ya majibu yao ni kama vile; "*Hukutana na marafiki njani", "Huchoka sana na kuchelewa kufika shule", "Nyumba ina mahitaji mengi hapa Tanzania".* Wengine waliandika methali mbalimbali zilizotumika kwenye kifungu cha habari na nyingine zilizoandikwa katika karatasi ya maswali kwa ujumla kama vile*: "Sikio la kufa halisikii dawa, kidole kimoja hakivunji chawa, shukrani ya punda ni mateke, mtaka cha uvunguni sharti ainame.* Kielelezo Na. 2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.


SWALI LA 41


i> Ukataji wa miti Umekuwa chanzo Kikubwa cha uharibifu wa mazingira

**Kielelezo Na. 2:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 41*

Kielelezo Na. 2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyenakili sentensi ya kwanza katika aya ya kwanza ya kifungu cha habari badala ya kuandika kichwa cha habari kama yalivyokuwa matakwa ya swali.


**Swali la 42:** Methali ipi yenye maana sawa na methali isemayo "sikio la kufa halisikii dawa?"

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika methali yenye maana sawa na methali "sikio la kufa halisikii dawa" kama ilivyotumika katika habari aliyosoma. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 25 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila alama.




**Chati Na. 25**: Asilimia ya watahiniwa katika kila alama


Chati Na. 25 inaonesha kuwa asilimia 48.39 ya watahiniwa waliojibu swali hili waliweza kuandika methali yenye maana sawa na methali husika. Watahiniwa hao waliandika kwa usahihi kati ya methali zifuatazo "*Asiyesikia la mkuu huvunjika guu, La kuvunda halina ubani, Asiyesikia la mkubwa hupata makubwa, au Asiyesikia la mkuu hufikwa na makuu*." Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali, hivyo kuweza kulinganisha na methali iliyotumika katika kifungu cha habari kwa usahihi. Kielelezo Na. 3 ni sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swali hili.




**Kielelezo Na. 3:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 42*

Hata hivyo, asilimia 51.61 ya watahiniwa walishindwa kuandika methali yenye maana sawa na methali "sikio la kufa halisikii dawa" iliyotumika katika kifungu cha habari. Baadhi yao waliandika methali tofauti na matakwa ya swali kwa mfano; *meno ya mbwa*

*hayaumani*, *baniani mbaya kiatu chake dawa*, *ngoja ngoja yaumiza matumbo*, na *haba na haba hujaza kibaba.* Wengine walinakili methali mbalimbali zilizokuwa katika maswali mbalimbali kama vile; *mchonga mwiko huukimbiza mkono wake, chanda chema huvikwa pete na asiyekubali kushindwa si mshindani.* Aidha, wapo walioandika mapendekezo mbalimbali kuhusu utunzaji wa mazingira. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika, "*kumshauri mtu na kutosikia* na *kumpeleka kwenye vyombo vya habari."* Majibu ya watahiniwa hao kwa ujumla hayakidhi matakwa ya swali hili. Kielelezo Na. 4 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.


SWALI LA 42


KUSIKILIZA KWA MAKINI

**Kielelezo Na. 4:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 42*

Kielelezo Na. 4 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa kauli yenye kutoa ushauri kwa kuzingatia methali "sikio la kufa halisikii dawa" badala ya kuandika methali yenye maana sawa na methali hiyo.


**Swali la 43:** Ni athari zipi zinaweza kumpata binadamu kutokana na ukataji wa miti ovyo? Taja athari mbili.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja athari mbili zinazoweza kumpata binadamu kutokana na ukataji wa miti ovyo. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 26 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila alama.




**Chati Na. 26**: Asilimia ya watahiniwa katika kila alama

Chati Na. 26 inaonesha kuwa asilimia 79.92 ya watahiniwa waliojibu swali hili waliweza kutaja athari zinazoweza kumpata binadamu kutokana na ukataji wa miti ovyo. Athari hizo ni kama vile, *kukauka kwa vyanzo vya maji na ukosefu wa mvua kwa muda mrefu.* Watahiniwa hao walitoa jibu hilo kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha ya kusoma habari na kufahamu maudhui yake kuhusu uharibifu wa mazingira. Kielelezo Na. 5 kinaonesha jibu sahihi la mtahiniwa katika swali husika.



SWALI LA 43

Kukauka kwa vyanzo vya maji.
Ukosefu wa mvua kwa muda mrefu.

**Kielelezo Na. 5:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 43*

Kwa upande mwingine, asilimia 20.08 ya watahiniwa walishindwa kutaja athari zinazoweza kumpata binadamu kutokana na ukataji wa miti ovyo kutokana na kukosa umahiri katika kusoma na kuelewa kifungu cha habari. Baadhi yao walibainisha shughuli mbalimbali za kibinadamu zinazofanyika katika mazingira yao mfano, *shughuli za kilimo katika bonde la Usangu, kilimo cha*

*mpunga Rufiji, kuchana mbao* na *kupata mkaa misitu ya hifadhi*. Watahiniwa wengine waliandika sababu za kuharibu mazingira mfano, kuchoma misitu ovyo na ukataji wa miti ovyo; majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 6 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali.


SWALI LA 43


(i) WATU WANA SHA URIWA KUPANDA MITI
(ii) KUACHA KUCHOMA MKA ANA NAKUCHOMA MAJANI PEMBEZONI MWA NYANZO YYA MAJI

**Kielelezo Na. 6:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 43*

Kielelezo Na. 6 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika ushauri wa mwandishi dhidi ya kutunza mazingira badala ya kutaja athari za ukataji miti ovyo kwa binadamu.


**Swali la 44**: Neno “beza” kama lilivyotumika katika habari uliyosoma lina maana gani?

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya neno “beza” kama lilivyotumika katika kifungu cha habari. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu. Chati Na. 27 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila alama.




**Chati Na. 27**: Asilimia ya watahiniwa katika kila alama


Chati Na. 27 inaonesha kuwa asilimia 75.87 ya watahiniwa waliojibu swali hili walishindwa kuandika maana sahihi ya neno *''beza''* kama lilivyotumika katika kifungu cha habari walichosoma. Baadhi yao waliandika athari za mazingira kwa binadamu mfano *kukauka kwa vyanzo vya maji* na *ukosefu wa mvua kwa muda mrefu;* Watahiniwa hao waliandika majibu hayo kutokana na tabia ya binadamu kubeza na kuharibu mazingira kumesababisha madhara hayo. Aidha, wapo watahiniwa walionakili aya ya mwisho kutoka kwenye kifungu cha habari mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kubeza ushauri huo unaotolewa na wataalamu wa mazingira na kuendelea na uharibifu*; na wengine waliandika majibu kama vile *adimu sana, kuomba ushauri, kumsema mtu* na *kuomba msaada*. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuelewa vyema maudhui ya kifungu cha habari, hivyo kushindwa kueleza maana ya msamiati huo kama ulivyotumika katika muktadha wa habari husika. Kielelezo Na. 7 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilo sahihi katika swali hili.




**Kielelezo Na.** 7: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 44*

Kielelezo Na. 7 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeeleza maana ya neno “beza” kuwa ni kutoa ushauri au kuongea badala kudharua au kupuuza.

Hata hivyo, asilimia 24.13 ya watahiniwa waliweza kujibu kwa usahihi swali. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msamiati “beza”. Hivyo, walitoa maana ya neno hilo kuwa ni *kudharau au kupuuza ushauri wa wataalamu kuhusu namna/jinsi ya kutunza mazingira* kulingana na muktadha wa habari husika. Kielelezo Na.8 kinaonesha jibu sahihi la mtahiniwa katika swali husika.



SWALI LA 44

Beza maana yake ni kudharau.

**Kielelezo Na.8:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 44*


**Swali la 45:** Funzo gani unalipata kutokana na habari uliyoisoma?

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,231 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika funzo alilolipata kutokana na habari aliyoisoma. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Chati Na. 28 inaonesha asilimia ya watahiniwa katika kila alama.




**Chati Na. 28**: Asilimia ya watahiniwa katika kila alama

Chati Na. 28 inaonesha kuwa asilimia 82.63 ya watahiniwa waliojibu swali hili waliweza kuandika kati ya mafunzo yafuatayo: *umuhimu wa kutunza mazingira, kupanda miti, kuacha kuchoma mkaa na kuacha kuchoma majani pembezoni mwa vyanzo vya maji*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa funzo stahiki kwenye kifungu cha habari walichopewa kwa kuwa waliweza kusoma na kukielewa vyema kifungu hicho. Kielelezo Na. 9 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa kufuata matakwa ya swali.



SWALI LA 45

Nimejifunzo kuwa nipande miti, niache kuchoma mkaa na kuchoma majani pembezoni mwa vyanzo vya maji.

**Kielelezo Na. 9:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 45*

Hata hivyo, asilimia 17.37 ya watahiniwa walishindwa kuandika funzo linalopatikana katika kifungu cha habari kwa usahihi. Baadhi yao waliandika majibu kama vile, *athari za mazingira, kukauka kwa vyanzo vya maji, ukosefu wa mvua kwa muda mrefu, kukata miti*

*kwa ajili ya mbao au kuni* na *kuchoma mkaa.* Majibu hayo ni shughuli zinazofanywa na binadamu zinazo athiri mazingira pamoja na madhara yanayotokana na shughuli hizo na sio funzo analolipata msomaji. Aidha, wapo watahiniwa ambao hawakuelewa matakwa ya swali kwani walinakili maelezo ya kichwa cha swali ambapo aliandika, *soma kwa makini habari ifuatayo kisha jibu maswali.* Wengine walinakili maswali kama ndio majibu yao kwenye swali husika. Uandishi wa majibu hayo unathibitisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa kifungu cha habari, hivyo kushindwa kubaini funzo lililomo katika kifungu cha habari walichosoma. Kielelezo Na. 10 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilo sahihi.




**Kielelezo Na. 10:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 45*

Kielelezo Na. 10 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyenakili methali iliyomo ndani ya kifungu cha habari badala ya kuandika funzo alilolipata kutokana na kifungu cha habari alichokisoma.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI

Umahiri uliotahiniwa katika somo la Kiswahili ni *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali*, kutumia *msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali, kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali, kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza, kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma,* na *kutumia msamiati katika kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali*.

Uchambuzi unaonesha kuwa, umahiri uliokuwa na kiwango cha juu zaidi ni *kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza (82.64%),* ikifuatiwa na *kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali*

(70.32%), *kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali* (61.82%), kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali (61.36) na *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali* (61.18%). Umahiri wa *kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma* ulikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 57.01.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, maswali matano kati ya maswali saba katika umahiri wa *kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza* yalijibiwa vizuri zaidi. Maswali hayo ni swali la 3 (92.91%), 1 (92.72.), 4 (91.94%), 5 (87.99%) na 2 (82.84). Katika umahiri wa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali*, swali la 17 lilijibiwa vizuri zaidi na kuwa na ufaulu wa asilimia (84.70). Aidha, swali la 10, 14 na 19 yalijibiwa vizuri ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 74.89, 82.18 na 70.46 mtawalia. Pia, katika umahiri wa *kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali,* maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi ni swali la 34 (81.94%) na 36 (81.55%). Katika umahiri wa *kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali,* swali la 22 ndilo lililojibiwa vizuri na kuwa na (72.50%). Vilevile, katika umahiri wa *kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma* swali la 43 na 45 yalikuwa na ufaulu wa juu zaidi wa asilimia 79.92 na 82.63 mtawalia. Aidha, katika umahiri wa *kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali,* swali la 28 lilikuwa na ufaulu wa juu wa asilimia 82.76 kuliko maswali mengine katika umahiri husika.

Viwango vya ufaulu katika mwaka 2023 vikilinganishwa na mwaka 2022 vinaonesha kuwa, katika umahiri wa *kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma,* kiwango cha ufaulu kimepanda kutoka asilimia 54.70 hadi asilimia 57.01; hivyo ufaulu umepanda kwa asilimia 2.31. Pia, katika umahiri wa *kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali*, kiwango cha ufaulu kimepanda kutoka asilimia 58.88 hadi 70.32 hivyo kupanda kwa asilimia 11.44. Vilevile, katika umahiri wa *kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo*

*alilosikiliza* ufaulu umepanda kwa asilimia 0.15 kutoka 82.49% hadi 82.64%. Hata hivyo, ufaulu umeshuka katika umahiri wa *kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali* kwa asilimia 1.81 kutoka 63.63% hadi 61.82%. Pia, katika umahiri wa *kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali*, kiwango cha ufaulu kimeshuka kutoka asilimia 77.97 hadi 61.36 sawa na asilimia 16.61. Vilevile, katika umahiri wa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali* ufaulu umeshuka kwa asilimia 0.54 kutoka 61.72 hadi 61.18. Kiwango cha ufaulu katika kila umahiri kimeoneshwa katika Kiambatisho Na. 1 na 2.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa umahiri unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili mwaka 2023 kilikuwa kizuri (65.72%). Vilevile, uchambuzi huu umebainisha changamoto zilizowafanya watahiniwa kushindwa kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi. Miongoni mwa changamoto hizo ni; kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu msamiati, nafsi mbalimbali katika vitenzi, upatanisho wa kisarufi na aina za maneno. Dosari nyingine ni kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo, au kutokujibu kabisa maswali.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu watumie mbinu ya kazi mradi, maigizo na bungua bongo kuwaongoza wanafunzi kujua maana na matumizi ya nahau na methali. Pia, wafahamu nafsi mbalimbali na mazingira ya utokeaji wake katika vitenzi ili kuwajengea uwezo na umahiri wa kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.

(b) Walimu wawaongoze wanafunzi kusoma kimya na kwa sauti kwa kuwaweka katika makundi na kujadili maudhui ya vifungu

vya habari au mashairi ili kuwajengea uwezo wa kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma.

(c) Walimu wawaongoze wanafunzi kufahamu aina za maneno kwa kutumia picha na vitu halisi, kadi zenye aina za maneno mbalimbali pamoja na igizo dhima kufafanua sifa za maneno na umuhimu wake katika sentensi. Hii itawajengea uwezo wa kutumia aina za maneno katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali.

(d) Walimu wawaongoze wanafunzi kufahamu msamiati mbalimbali, kubadili vitenzi kuwa nomino na kuunda maneno kutokana na silabi zilizochanganywa kwa kutumia njia shirikishi kama vile, kuwaweka wanafunzi katika vikundi na kuwasilisha kazi mbele ya darasa, kusoma matini mbalimbali pamoja na kutumia bungua bongo. Hii itawafanya wanafunzi kuwa na umahiri wa kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali.

(e) Walimu wawaongoze wanafunzi kufahamu kusikiliza habari au hadithi fupi kwa kutumia njia shirikishi ya kukaa katika vikundi. Mwalimu atawasomea habari/hadithi na mwisho atawauliza maswali juu ya walichosikiliza. Hii itawajengea uwezo wanafunzi wa kusikiliza kwa makini na kuonesha uelewa wa matini waliyoisikiliza.

(f) Walimu katika mitihani yao ya ndani (majaribio ya wiki, mwezi na mitihani ya kufunga mihula) watunge maswali yanayopima umahiri wa wanafunzi kwa kuzingatia mihtasari ya masomo husika. Maswali yatakayotungwa yapime nyanja zote za utambuzi ambazo ni ; kukumbuka, kuelewa, kuchambua, kutumia, kutathmini na kuunda. Aidha, wanafunzi wapewe mrejesho kuhusu matokeo ya upimaji huo ili kuboresha mchakato mzima wa ujifunzaji na upimaji darasani.

**KIAMBATISHO NA. 1**

## UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA UMAHIRI KATIKA PSLE 2023

| Na | Umahiri | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza. | 1 | 92.72 | 82.64 | Vizuri |
| | | 2 | 82.84 | | |
| | | 3 | 92.91 | | |
| | | 4 | 91.94 | | |
| | | 5 | 87.99 | | |
| | | 6 | 78.95 | | |
| | | 7 | 51.16 | | |
| 2. | Kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali. | 26 | 73.9 | 70.32 | Vizuri |
| | | 27 | 61.98 | | |
| | | 28 | 82.76 | | |
| | | 29 | 78.49 | | |
| | | 30 | 54.5 | | |
| 3. | Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali. | 20 | 55.99 | 61.82 | Vizuri |
| | | 21 | 66.87 | | |
| | | 22 | 72.5 | | |
| | | 23 | 59.25 | | |
| | | 24 | 67.97 | | |
| | | 25 | 48.38 | | |
| 4. | Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. | 34 | 81.94 | 61.36 | Vizuri |
| | | 35 | 63.52 | | |
| | | 36 | 81.55 | | |
| | | 37 | 60.56 | | |
| | | 38 | 72.78 | | |
| | | 39 | 35.87 | | |

| Na | Umahiri | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| | | 40 | 33.36 | | |
| 5 | Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali. | 8 | 66.17 | 61.18 | Vizuri |
| | | 9 | 49.79 | | |
| | | 10 | 74.89 | | |
| | | 11 | 50.82 | | |
| | | 12 | 49.55 | | |
| | | 13 | 53.02 | | |
| | | 14 | 82.18 | | |
| | | 15 | 47.06 | | |
| | | 16 | 53.31 | | |
| | | 17 | 84.7 | | |
| | | 18 | 52.31 | | |
| | | 19 | 70.46 | | |
| 6 | Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma | 31 | 37.43 | 57.01 | Wastani |
| | | 32 | 52.74 | | |
| | | 33 | 55.01 | | |
| | | 41 | 75.83 | | |
| | | 42 | 48.39 | | |
| | | 43 | 79.92 | | |
| | | 44 | 24.13 | | |
| | | 45 | 82.63 | | |

**KIAMBATISHO NA.2**

## ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA UMAHIRI KATIKA PSLE 2022 NA PSLE 2023

| Na | Umahiri | Mtihani wa 2022 | | | | Mtihani wa 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza. | 1 | 85.68 | 82.49 | Vizuri | 1 | 92.72 | 82.64 | Vizuri |
| | | 2 | 82.17 | | | 2 | 82.84 | | |
| | | 3 | 90.39 | | | 3 | 92.91 | | |
| | | 4 | 80.81 | | | 4 | 91.94 | | |
| | | 5 | 86.47 | | | 5 | 87.99 | | |
| | | 6 | 73.74 | | | 6 | 78.95 | | |
| | | 7 | 78.17 | | | 7 | 51.16 | | |
| 2. | Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma. | 31 | 59.94 | 54.7 | Wastani | 31 | 37.43 | 57.01 | Wastani |
| | | 32 | 64.35 | | | 32 | 52.74 | | |
| | | 33 | 41.56 | | | 33 | 55.01 | | |
| | | 41 | 22.03 | | | 41 | 75.83 | | |
| | | 42 | 65.76 | | | 42 | 48.39 | | |
| | | 43 | 30.36 | | | 43 | 79.92 | | |
| | | 44 | 82.42 | | | 44 | 24.13 | | |
| | | 45 | 71.19 | | | 45 | 82.63 | | |
| 3. | Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali. | 20 | 40.79 | 63.63 | Vizuri | 20 | 55.99 | 61.82 | Vizuri |
| | | 21 | 53.67 | | | 21 | 66.87 | | |
| | | 22 | 59.53 | | | 22 | 72.5 | | |
| | | 23 | 86.5 | | | 23 | 59.25 | | |
| | | 24 | 63.99 | | | 24 | 67.97 | | |
| | | 25 | 77.31 | | | 25 | 48.38 | | |

| Na | Umahiri | Mtihani wa 2022 | | | | Mtihani wa 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 4. | Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. | 34 | 73.96 | 77.97 | Vizuri | 34 | 81.94 | 61.36 | Vizuri |
| | | 35 | 82.32 | | | 35 | 63.52 | | |
| | | 36 | 83.66 | | | 36 | 81.55 | | |
| | | 37 | 77.55 | | | 37 | 60.56 | | |
| | | 38 | 77.6 | | | 38 | 72.78 | | |
| | | 39 | 74.14 | | | 39 | 35.87 | | |
| | | 40 | 76.57 | | | 40 | 33.36 | | |
| 5. | Kutumia msamiati katika kusoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali. | 26 | 61.38 | 58.88 | Wastani | 26 | 73.9 | 70.32 | Vizuri |
| | | 27 | 43.06 | | | 27 | 61.98 | | |
| | | 28 | 55.54 | | | 28 | 82.76 | | |
| | | 29 | 77.31 | | | 29 | 78.49 | | |
| | | 30 | 57.31 | | | 30 | 54.5 | | |
| 6. | Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali. | 8 | 82.15 | 61.72 | Vizuri | 8 | 66.17 | 61.18 | Vizuri |
| | | 9 | 56.1 | | | 9 | 49.79 | | |
| | | 10 | 65.09 | | | 10 | 74.89 | | |
| | | 11 | 71.99 | | | 11 | 50.82 | | |
| | | 12 | 61 | | | 12 | 49.55 | | |
| | | 13 | 57.38 | | | 13 | 53.02 | | |
| | | 14 | 49.62 | | | 14 | 82.18 | | |
| | | 15 | 71.59 | | | 15 | 47.06 | | |
| | | 16 | 62.22 | | | 16 | 53.31 | | |
| | | 17 | 55.52 | | | 17 | 84.7 | | |
| | | 18 | 78.45 | | | 18 | 52.31 | | |
| | | 19 | 29.62 | | | 19 | 70.46 | | |